ALHAMISI

Alikubali kukutana nami siku ya Alhamisi. Sikuamini na sikutarajia. Kusema kweli haikuwa rahisi kumshawishi kukubali kukutana nami na ilinichukua muda kumhakikishia kuwa sikuwa napanga jambo baya kwake. Nilipompigia simu jana yake wakati narudi nyumbani baada ya kumkosa kwenye kibanda chake kule mjini kitu cha mwisho kabisa nilichotarajia kilikuwa ni yeye kupokea simu mara moja. Nilikuwa nimejiandaa kuzungumza naye ana kwa ana kuliko kuzungumza kwa njia ya simu. Hicho ndicho kilichonifanya kujikute koo limenikauka na maneno yamenipotea kama mvuke. Nakumbuka vizuri jinsi nilivyojaribu kuishika simu vizuri mkononi ili isije kuniponyoka pale alipoipokea na kuniita "*hallow"*

Alipoita tena mara ya tatu "*Hallow*" ndipo nilishusha pumzi na kujibu kwa sauti iliyokatika kama ya mtoto aliyegutushwa akifanya kitu ambacho hakutakiwa kufanya.

"*Hallow*" Nilijibu.
"*Hallow*, nani mwenzangu"? aliniuliza yawezekana alishajua ni nani lakini alitaka tu kuwa na uhakika aliyekuwa upande wa pili ni nani.
"Una wenzako wangapi wanaokutukana hadharani" nilisema kwa utani kidogo. Alikaa kimya kwa sekunde. Moyo ulinilipuka na mara moja nilijua nimetumia utani mbaya na anaweza kunikatia . Nilijilaumu kwa kujifanya mchekeshaji.
"Hahahaha, dada Clementina; Shikamoo dada" alijibu akitangulia na kicheko. Moyo ulitua na kutulia. Kicheko chake kilinifariji kuwa angalau anajua utani. Nilisema moyoni "*thank you Jesus*" utadhani vile vibibi vya Wamarekani weusi kwenye filamu zao. Nikatabasamu.

"Jamani, mbona unanizeesha wewe; niite Clementina au Tina tu ukipenda" nilisema na kuitolea nje kiaina hiyo shikamoo yake. Moyoni nikamuuliza *unaniita dada nikikupa utakataa?*

"Sawa dada Tina, kwa kweli samahani sana kwa yaliyotokea juzi" alianza kuniomba msamaha. Sikutegemea angerudia tena kufanya hivyo. Mara moja donge la uchungu lilinikaba tena kooni. Jamani huyu kijana alikuwa *'unbelievably"* mwema wa kushangaza. Yaani, mimi ndio nimepiga simu kumuomba msamaha lakini yeye akaniwahi tena. Angekuwa karibu ningejirusha mikononi mwake nimpe busu la kunyong'onyea mbele yake.

"Freddy, kwa kweli mimi ndio napaswa hasa kukuomba msamaha" niliamua kumkatisha na kuingiza msamaha wangu. "Lakini sasa hivi niko barabarani ningependa tuonane ili nikutake radhi uso kwa uso kwa makosa yangu ya Jumatatu" nilimuambia. Nilisubiri akubali tu mara moja ili nikate simu kabla hajabadili mawazo. Lakini nilikuwa nahofu asingeweza kukubali kirahisi hivyo.

"Mmh…" aliguna. Sikujua kwanini ameguna au alikuwa anafikiria nini.

"Au unasemaje Freddy" nilimuuliza kwa sauti ya unyonge kama ninayebembeleza. Unajua wakati mwingine wanawake tuna sauti ambayo tukiitumia huweza kupata tunachotaka hata kwa jambazi lililokubuhu.

"Kwa kweli sijui, Tina wewe ni mke wa Waziri uje ukutane na mimi; *I'm nobody. I don't understand why you would want to meet me- a person of your status. It doesn't make any sense at all Tina*" alisema kwa Kiingereza safi hadi nikajisikia kutekenyeka sehemu ambazo siwezi kuzisema! Kijana lugha ilikuwa inapanda siyo kile cha kuombea maji kama nilivyodhani.

Nikaamua na mimi kwenda katika Kiingereza.

“Mimi si mke wa Waziri bwana” niliamua kumdanganya kwani nilijua tayari hiyo itakuwa issue. “Kwanza nani kakuambia hivyo jamani wamekutisha tu” nilisema na kujaribu kumuondolea hofu. Sikutaka kabisa ndege wangu anikimbie au aniogope kwa sababu mimi ni mke wa Waziri.

“One guy told me that the other day” akajibu tena kwa kiingereza. Nikamkumbuka yule jamaa aliyemnong’oneza wakati wa mgongano wetu Jumatatu. Nilimlaani kwa lugha zote za kuzaliwa na za kukulia kwa kujaribu kunifukuzia tetere wangu.

“*Its not true, I get that all the time somebody would always confuse me with a wife of some Minister in the government”* nilimuambia. Sikujua kama ilikuwa sawa kumwambia hivyo au ningemwambia tu ukweli yaishe. Niliamua kumdanganya. Nilijisikia vibaya lakini lililopaswa kufanywa lilifanywa.

“Kwa hiyo siyo mke wa Waziri?” aliniuliza sasa kwa Kiswahili. Safari hii sauti ilikuwa imechangamka kama kwa matumaini fulani.

“No, I’m not” nilijibu kwa Kiingereza. Na nikaendelea kwa kimombo *“ Freddy, I really would like to meet you because the first meeting was not a very good one and had left me with a very guilty conscious and negative feelings all these few days*” nilimuambia kwa kuyapanga maneno hayo kwa taratibu na kuyatamka kwa mapozi utadhani niko kwenye mashindano ya kupanga herufi. “Kwa hiyo, nitafurahi kama utanipa nafasi ya kukutana nami” niliweka kituo na sikio langu likisubiri kusikilizia jibu lake.

Alichukua muda kidogo kufikiria. Sekunde hizo chache zilikuwa kama milele. Macho yangu yalikuwa yanaangalia mbele barabarani huku mdomo wangu nimeuuma kwa hofu ya kukataliwa.

“Wapi?” aliniuliza. Sasa hapo ndio kichekesho kingine kikanipata. Sikuwa nimefikiria wala kutarajia kuwa atakubali kirahisi hivyo; sikuwa nimefikiria wapi tunaweza kukutana. Muda haukuwa tatizo kwani Alhamisi sikuwa na mambo mengi na Waziri alikuwa ametingwa na shughuli za maandalizi ya Siku Kuu ya Muungano. Sasa aliponiuliza “wapi” kwa kweli nilikuwa zero kabisa kichwani, *sifuri*, *nyet*. Maeneo yote ninayoyajua mimi ni maeneo ambayo nimekuwa nikienda na mume wangu au na kina mama wengine mashuhuri ambayo kwa kweli najulikana nikionekana uso tu. Nilijua siwezi kwenda sehemu hizo na kwa hakika nisingeweza kumleta nyumbani kwangu. Akili yangu ilianza kwenda mbio utadhani daladala linalowahi wateja kabla hawajachukuliwa na mwingine.

“Duh.. Freddy kwa kweli hata sijafikiria mbali hivyo, unaweza kunishauri” nilikiri nikiunganisha na kicheko cha wasiwasi na kumuacha aamue pa kukutania. Akaniuliza ninakoishi na nilimwambia Mbezi ya Kimara. Kwa mara nyingine tena sikutaka kumuambia ukweli. Sasa mtu anaweza kunihukumu lakini niliona ni bora nisimuambie mwanzoni ili asije akawa na wasiwasi zaidi au akakosa kuwa mtulivu. Nilitaka nimpe nafasi ya kunijua mimi bila vikolokolo vingine vya maisha yangu.

“Ah, unafahamu ilipo Blue Pearl?” Aliniuliza. Nilikiri kupajua kwani ni mahali ambapo ninapita mara kwa mara.

Asubuhi ya Alhamisi haikuwa na vurugu zozote na mzee hakuwa na usumbufu wowote. Alirudi jana yake akiwa amechoka na alinikuta nishaenda kulala. Alfajiri niliamka mapema kama kawaida na kufanya kazi za ofisi pale ndani na kwenda kumuandalia kifungua kinywa mzee. Hata hivyo siku hiyo niliamka na mawazo yangu yote yakiwa yanaangalia saa nane. Kila nikifirikia mwili ulinisisimka.

Akinigusa itakuwaje.

Hayo mawazo yalikuwa yananijia kama kwa vipimo. Kila nikijaribu kufanya mambo yangu ya hapo nyumbani utadhani mtu ananinong'oneza.

Utajisikiaje akikubusu shingoni?

Hadi inafika kama saa tano za asubuhi nilikuwa nimebadili chupi yangu mara tatu. Nilikuwa najilowesha kwa mawazo machafu (na matamu) sijui kwa kitu gani. Sijawahi kutekwa katika hisia za mapenzi na ngono kama ilivyokuwa asubuhi hiyo. Nikifikiria macho yake, sauti yake ambayo kila neno alilotamka jana kwenye simu lilikuwa kama wimbo usiokoma katika mawazo yangu. Kuna wakati hapo nyumbani asubuhi hiyo nilipoteza sekunde chache nikiwa nimesimama nimezama kwenye mawazo ambayo kwa ufupi yalikuwa ni ya mimi na Mjamaika wangu.

Kwa kadiri saa zilivyokuwa vinakwenda ndivyo na mimi moyo ulivyokuwa unazidi kwenda kasi. Ilipofika saa sita nilikuwa tayari nimeshaoga na kuwa tayari kutimka hapo nyumbani. Kusema ukweli siku hiyo sikuwa na ujanja isipokuwa ilinipasa kujiweka vizuri. Nilitaka kutuma ujumbe kuwa akitaka atapewa. Lakini vile vile hata asipotaka atapewa tu!

Nilivaa suruali ya kahawia iliyoiva iliyokuwa inapwaya miguuni lakini iliyobana kile alichonipa mama yangu! Nilidokeza awali kuwa nimejaliwa matako; siyo ya vurugu au kumwaga lakini yalikuwa kama kitunguu cha Tukuyu. Yalikuwa ni mduara nusu mzuri na yalifichua kiuno changu chembamba kwa wastani. Mwenyewe sikuwa mwembamba hivyo ila urefu wangu na mwili wangu unaweza kusema kwa urahisi tu kuwa nilikuwa nina mwili wa wastani. Nilivaa tsheti ya rangi ya maziwa iliyopauka ambayo ilikuwa na maua yaliyozungushwa zungushwa ya rangi ya kahawia kali. Hiyo tisheti ilikibana kifua changu vizuri na kuhakikisha kuwa matiti yangu yalikuwa yamefichwa vizuri lakini yakibakia kuchombezwa. Nisingeweza kupita mahali bila mtu kuangalia kifuani na kutamani kujua kilicho nyuma yake. Nilivaa viatu virefu vya wastani vya rangi ya maziwa vile vile. Sikutaka kuvaa hereni lakini nilivaa mkufu wa dhahabu wenye kidani cha msalaba mdogo uliong'ara. Kusema ukweli nilipodoa. Sikutaka kuondoa hivyo hivyo tu nikaongeza juu yake na kitambaa ambacho nilikiangushia mabegani. Kwenye mkoba wangu nilibeba vitu vya kawaida ikiwemo kanga ambayo kwa mwanamke wa jiji la Dar ni muhimu sana kuwa nayo karibu; huwezi kujua utaihitaji katika mazingira gani.

Niliondoka muda huo wa saa sita kuelekea Blue Pearl Hotel. Sijui barabara ya Morogoro ina vitu gani lakini kutoka nyumbani hadi nafika maeneo ya Bunge nilikutana na ajali tatu ambazo hakuna hata moja ambayo ungeweza kumueleza mtu ilivyotokea akaelewa. Hizo ajali zilinichelewesha kidogo na kunifanya nifike pale saa nane na robo. Niliegesha gari langu kwenye maegesho yao.

Kwa kweli hoteli hii ni miongoni mwa hoteli zenye mvuto wa ajabu kuanzia unavyoingia eneo hilo. Sijawahi kufika hapo lakini kwa mara yangu hiyo ya kwanza nilifurahi kuwa nakutana na Mjamaika wangu hotelini hapo. Nembo yake ya taji lenye lulu ya rangi ya bluu ndani yake ilinialika hapo nami nikakaribia. Nilipofika ndani nilielekezwa ulipo mgahawa wao. Haikunichukua muda niliona mtu ananipungia mkono kwenye kona iliyokuwa inaangalia liliko bustani nzuri ya maua ambapo watu huketi nyakati za jioni kupata nyama choma. Mjamaika alikuwa ameshafika. Mwenzenu miguu ilitetemeka, nilijihisi nadhoofika ghafla. Tabasamu lake la kutoka mbali kwangu lilikuwa kama sumaku. Nilivutwa na moyo wangu ukanaswa.

Nilielekea alikokuweko kwa mwendo wa mahesabu, mkoba mkononi, kitambaa kikiangukia mabegani, ufunguo wa gari nimeufumbata mkono wa kushoto. Alikuwa amechagua sehemu ya

kwenya kona nzuri na hivyo ilitupa nafasi ya kuangalia eneo zima la mgahawa wa hoteli hiyo. Niliweza kuona wageni wakiingia na kutoka hotelini hapo na kupafanya mahali hapo kuwa pamechangamka kweli. Bila ya shaka wengi ni wafanya biashara au wasafiri maana hoteli yenyewe haiko mbali sana na kituo cha mabasi ya kwenda mikoani.

“Habari yako Freddy” nilimsalimia.
“*Hi Tina, how are you*” alinijibu akiwa bado amesimama. Alinyoosha mkono wake kunisalimia, raha juu ya raha. Hakuwa amevaa kofia yake ya kirasta bali alizifunga nywele zake nyuma na kuziacha ziangukie mgongoni. Kinyume na marasta wengi huyu alizitengeneza nywele zake vizuri kweli na zilikuwa zinang’ara kwa mafuta. Alikuwa amekata ndevu zake kwa mtindo wa “o” ambayo ilifichua midomo yake ya rangi nyeusi. Nilitarajia atavaa mojawapo ya mavazi yake ya *kijah people* lakini alikuwa amevaa suruali nyeusi na shati jeupe la mikono mirefu. Shati lilikuwa na mifuko miwili mikubwa mbele, ule wa kushoto ulikuwa na kalamu ya rangi ya fedha ikitokezea shingo yake tu. Sijui alitumia manukato gani lakini yalinivutia mno.
“Umependeza” aliendelea bila ya kunipa muda kuendelea kumfikiria. Sijui ni kitu gani ambacho wanawake tunacho wakati mwingine lakini mwanamme anavyotokea huwa tunapenda sana kujaribu kuangalia kila kitu tuone kama kiko perfect. Wakati mwingine inaudhi kwa sababu unajikuta unaanza kumkosoa mawazoni na kutamani angekuwaje au angevaaje. Mbele ya Mjamaika wangu (nafahamu ni Mluguru, lakini daima atakuwa Mjamaika kwangu) sikutaka kukosoa lolote kwani alikuwa “perfect”.
“asante na wewe umependeza” nilirudisha sifa. Alinivutia kiti upande mmoja na kunisubiri niketi kisha akaenda upande mwingine wa meza na kuvuta kiti chake na kuketi tena. Tuliangaliana machoni kwa sekunde.
“Una njaa” aliniuliza. Huyu kijana sijui *vipi.* Nilijiwazia.

“Kwa kweli nina njaa” nilisema na kucheka. Mara moja alipunga mkono na mhudumu akaja kuchukua order zetu. Muda wote huo akili yangu ilikuwa inazunguka kama pia kichwani mwangu. Alikuwa na sauti ya upole na ya kubembeleza na pia kakamavu sana. Ningetamani alale pembeni yangu huku akizungumza nami usiku kucha. Nisingechoka kumsikiliza.

“Tina kwa kweli sielewi kwanini umenitafuta namna hii” alianza kusema huku akiniangalia machoni. Macho yake yalikuwa kama gololi angavu, yalimulika mulika utadhani yamewekwa utepe wa mafuta. Niliyakwepa kwani niliona yanaweza kusoma mawazo yangu yote machafu.
“Hata mimi sielewi bwana” nilisema na sauti nikailegeza. Nilijiuma mdomo kidogo.
“Unajua kabisa kuwa mambo kama yale ya Jumatatu hutokea na hukuwa na sababu ya kuniomba msamaha” aliniambia.

“Hapana, nilikuwa na sababu.Sikupaswa kutahamaki vile, ningechukulia tu kuwa ni ajali” nilisema kwa msisitizo.

“Niambie ukweli Tina, kwanini ulihamaki vile yaani sikuelewa na nafikiri hicho ndicho kilichonisumbua” alisema kwa sauti ya upole ambayo ilikwepa kunibebesha mashtaka au lawama. Nilikosa maneno. Nilitamani nimsimulie matatizo niliyonayo na mume wangu, na jinsi ambayo kwa muda mrefu nimekaa mbali na wanaume. Nilitaka nimsimulie msongamano wa mawazo juu ya maisha na upweke nilio nao moyoni. Sikuthubutu.
“Mimi sijui lakini nilijisikia vibaya tu nilipoondoka na nikajilaumu kwani unaonekana ni kijana mzuri na sikukutendea haki, naomba unisamehe kweli” nilisema machozi yakinilenga. Sikutarajia alichofanya baada ya hapo. Aliivuta mikono yangu juu ya meza na akaiweka ndani ya mikono yake. Uso wake aliuinua na kuniangalia machoni. Moyo ulishtuka na kupigwa na hamasa. Mguso wake

ulikuwa ni mguso wa umeme kwenye mti ulioloa; vidole vyake vilipogusa mikono yangu nilijihisi nimeguswa na malaika (touched by an angel). Sikutaka aniachie.
“Usiwe na shaka nimekusamehe Tina, na ya kale yamepita tugange yajayo” aliniambia na kuiminya mikono yangu kidogo. *Halleluya!* Nilimuangalia machoni kwa nukta chache, niliinamisha kichwa changu kwa haya na kucheka kwa aibu. Aliihurumia mikono yangu na kuniachilia.
“Nini tena” aliniuliza kwa mshangao.
“Siamini kwamba nimekaa na wewe hapa” nilimjibu nikilegeza zaidi sauti. Wakati mwingine wanaume wanafikiri huwa tunalegeza sauti kwa makusudi, si kweli. Wakati mwingine sauti inajilegeza yenyewe ikiwekwa kwenye usawa wa kati. Nilisikia kijasho chembamba kikitirika kwapani. Joto la mwili lilianza kunipanda.
“Hata mimi, kusema ukweli ile Jumatatu uliniacha na hisia zimechanganyika sana, ulinivutia lakini wakati huo huo ulinifukuza” alisema. Na nilielewa anamaanisha nini. Aliendelea kunieleza kuwa hakuelewa kwanini mwanamke ambaye kwa kila kipimo alionekana mwenye staha na heshima zake kuwa kama mtu aliyejeruhiwa. Alitamani aweze kuniita chemba na kuyamaliza kama watu wazima lakini asingeweza kwani nilikuwa kama mbogo aliyejeruhiwa. Nilisikitika na kumuomba tena samahani. Mhudumu alileta vyakula tulivyoagiza.
Tulianza kula taratibu nakuzungumza mambo mbalimbali kuanzia hoteli ya Blue Pearl na jinsi gani ingeweza kuboresha zaidi mambo mbalimbali kwani kwa kuangalia kwa nje tu ilikuwa ni nzuri sana. Alinisimulia baadhi ya matatizo ya huduma lakini alisema kwa kweli ni hoteli ambayo inajitahidi sana. Tulipomaliza kula tulikuwa tumeanza kuzoeana utadhani tuliofahamiana miaka. Tulikuwa tunacheka na kuchekeana. Niseme wazi kuwa kulikuwepo na *chemistry* ya kiwango cha juu kati yetu. Kwa kadiri tulivyotazamana na kutaniana ndivyo macho yetu yalivyokuwa yakizidi kunong’onezana katika lugha ambayo nimacho tu yanaweza kuelewa. Kuna namna aliyoniangalia midomo yangu au kifuani iliyonifanya niwaze tu “sema utapewa”.
“Mke wako akikukuta hapa si itakuwa kasheshe?” nilimuuliza. Sikutaka kumuuliza swali ambalo nilitaka hasa kumuuliza.
“Unaniuliza kama nina mke?” aliniangalia machoni. Nusura nikimbie. Nilimuitikia kwa aibu kwani nisingeweza kumuuliza moja kwa moja.
“Sina mke wala sina mtu kwa sasa” alisema na kujibu swali la pili yake ambalo ningemuuliza. Aliniambia kuwa ana mtoto mdogo wa miaka sita ambaye anaishi naye pamoja na wadogo zake wawili wa kike na wa kiume. Mama wa mtoto waliachana zamani na yeye aliachiwa mtoto. Aliniambia ametoka kwenye mahusiano mabaya hivi karibuni na kwa wakati huu ameamua kuwa “mapumzikoni” akitilia mkazo biashara zake na mambo yake yeye mwenyewe. Nilimuonea huruma. Alizungumza kama mtu ambaye bado alikuwa ana uchungu moyoni, nilitamani niwe pale kumpa faraja.
“Umeniambia siyo mke wa Waziri lakini naona umevaa pete ya ndoa” aliniuliza. Nilikiri kuwa nilikuwa nimeolewa lakini pia wakati huo na mimi naenda kwenye mahusiano mabaya na changamoto kubwa kwenye ndoa. Tukaanza kuzungumza na sikutaka kumficha nilimueleza ukweli wa umbali uliopo kati yangu na mume wangu ambaye nilimuambia tu kuwa ni Daktari.
“Pole sana Tina” aliniaambia baada ya kumsimulia kisa changu. Kwa mara nyingine tena alinishika mikono yangu na kunipa faraja.
“Sijui ni kitu gani kimenivuta kwako Freddy, lakini umeniingia mawazoni sana tangu Jumatatu” nilikiri na kuamua kuweka karata zangu mezani. Nilimueleza (bila kumpa utamu wote) kuwa tangu nilipomuona nilitamani nifahamiane naye zaidi na hata kuwa marafiki.
“Hahahah, yaani urafiki wa kaka na dada au” aliniuliza kwa mtego. Nilijua ndoana nimerushiwa na ilikuwa ni uamuzi wangu kunasa. Niliamua kunasa.
“mmh.. inategemea wewe unataka nini” nilimrudishia kama pasi ya mpira.

“Kama nilivyokuambia natoka kwenye uhusiano mbaya na sijui kama niko tayari kuanza mahusiano mengine” aliniambia. Moyo uliniuma na uchungu ulipasua mifupa yangu. Freddy naona alikuwa ananichomoa. Nilijisikia mjinga na nilijilaumu kufikiria kuwa angeweza kuukubali moyo wangu hivyo.
“lakini” aliendelea, “sitojali kukufahamu zaidi na kama lolote tutakalotaka liwe likawa sitajilaumu” aliniambia. Nusura nilie. Hakunikataa moja kwa moja lakini alinipokea kwa uangalifu wa moyo. Nilifurahi.
“Freddy, sijui kwanini lakini kwako najisikia niko comfortable kweli” nilikiri na kuangusha kicheko. “Ni kama nakufahamu kwa muda mrefu” nilimuambia. Aliniangalia machoni na macho yote yaliendelea kunong’onezana maneno matamu na ya raha. Ni kama alikuwa ananitumia ujumbe ambao ni moyo wangu tu uliweza kuulewa. Mara miguu yetu chini ya meza ikagongana kidogo, tukajikuta wote tumeanza kucheka. Mezani vyombo vilikwisha ondolewa na tukabakia na vinywaji tu. Upande ambao tulikuwa tumekaa kama nilivyosema ilikuwa ni kwenye kona, mimi nilikuwa niko upande unaoangalia ukumbi mzima hadi wanakoingilia wageni wakati yeye alikuwa amewapa mgongo.
“Njoo ukae pembeni yangu basi” alinialikia.
“Nikae hapo” nilimuuliza huku nikiashiria kwa kichwa. Kwa wakati wote huo tulikuwa tumekaa kama watu tu ambao wanapiga stori na bila ya kuonesha ukaribu wowote ule. Alivyonikaribisha nikae pembeni yake nilisikia raha.
“Sitaki kuzungumza kwa nguvu bwana” aliniambia. Niliacha kitambaa na mkoba upande ule wa meza nikahamia upande wake. Alinipisha na kunipa nafasi ukutani. Mtu akiingia kutoka nyuma yetu asingeweza kuona kama kuna mtu wa pili na hakukuwa na meza zaidi yetu. Tuliweza kuangalia bustani nzuri ya Blue Pearl na watumishi mbalimbali walionekana kuiandaa kwa shughuli za jioni hapo kwani watu hupenda kuketi hapo nje jua likitua kwa ajili ya nyama choma na kuteremshia na vinywaji baridi. Madirisha yalikuwa na rangi iliyozuia watu wa nje kuona ndani lakini walio ndani kuona nje bila kuumiza macho yao katika mwangaza wa jua.
“Tina, sijui kwanini umekuja katika maisha yangu leo hii” alianza kusema “lakini vyovyote vile ilivyo ninafurahia ulinitatufa” alisema huku akiniangalia nikiwa nimeketi pembeni yake. Miili yetu iligusana kidogo na raha niliyojisikia hakuna maneno yanayotosha kuelezea.
“Hata mimi Freddy, asante kwa kukubali kuja” nilimuambia niliangusha macho chini kwa aibu za Kichagga.
“Usiwe na wasiwasi, tutakuwa pamoja inavyowezekana” aliniambia. Mkono wake wa kushoto aliuweka kwenye paja langu. *Mama yangu*! Sijui kama alikuwa anajua anachonifanyia mwilini mwangu. Nilijisikia raha niliuteremsha mkono wangu na kuuweka juu ya wake na kumzuia kuundoa mkono wake. Nilitaka ukae hapo kwa dakika chache zaidi ili nijisikilizie. Nilicheka tu kidogo.
“Mbona unatetemeka” aliniuliza. Sikujua nilikuwa natetemeka. Miguu yangu ilikuwa inatetemeka, vidole vyangu vilikuwa vinatetemeka.
“Sijui kwanini bwana” nilimuambia.
“Pole, mbona inakuwa kama siku nyingi zimepita toka uwe na mtu namna hii?” aliniuliza kama daktari aliyejua dawa ya kunitibu ugonjwa wangu. Aliniuliza huku macho yake yakiniangalia kwa kuchombeza.
“Kweli siku nyingi, yaani hapa nilipo niko hoi Freddy” nilimuambia.
“Oh yeah?” aliuliza.
“Sijui ni kitu gani kimeniingia kwako, siamini niko hapa, na siamini kila kinachoendelea” niliamua kumuambia ukweli huo. Aliutoa mkono wake na kuuweka mgongoni kwangu. Alianza kunizoea, na nilipenda anizoee hivyo. Mkono wake mgongoni ulikuwa kama mkono wa mpenzi wa muda mrefu. Nilisikia raha mgongoni kama umeme ukipita kwa kasi hadi kiunoni. *Itabidi nibadili tena chupi yangu!* Nilikuwa nimelowa tena chapachapa.
Alirudisha mkono wake kwenye paja langu. Nilitingisha miguu yangu kwa msisimko. Aliuzungusha mkono wake kiunoni mwangu

chini ya tisheti yangu. Nilifumba macho kwa sekunde. Joto lilizidi kunipanda. Nilicheka kwa sauti ya chini. Sikujaribu kumzuia. Vidole vyake vilifika kwenye vifungo vya suruali yangu vilivyokuwa pembeni kidogo. Kimoja kimoja alianza kukiachia. Ooh my goodness, I hope he is not going to do *that!* Nilijiambia. Nilinyosha mkono na kuvuta mkoba wangu toka upande ule na kuuleta karibu yangu. Vifungo vyote viliachia.
Freddy alijua anachotaka kufanya; kama jasiri asiyeogopa kitu aliingiza mkono wake ndani ya suruali yangu na kunipapasa taratibu juu ya chupi yangu. Aliweza kuhisi unyevu nyevu.
“Oh lalah” alilalamika kwa raha.
“Jamani usiache” nilimuambia maana nilihisi anaweza kuacha. Nilibana miguu yangu baada ya kunigusa kwa namna fulani. Nusura nipige kelele.
“Sina mpango wa kuacha darling” alinihakikishia. Alirudisha vidole vyake hadi juu kidogo na taratibu aliviingiza chini ya chupi yangu, ninaposema taratibu nina maana hakuwa na vurugu, nilikuwa nimeganda utadhani nimemwagiwa maji ya baridi. Nilichukua kanga iliyokuwa kwenye mkoba na kuiweka juu ya mkono wakemikono yangu yote miwili niliiweka juu ya meza, niliinama kidogo kuegamia meza na kiuno nikakirudisha nyuma. Nilijisikilizia. Sijui alijifunza wapi lakini alilichanua waridi langu kwa ufundi na hakufanya nilivyotarajia. Nilidhani atachomeka kidole ndani; alipapasa malango ya hekalu langu, na kwa kidole chake taratibu alinipapasa kwenye kinembe changu akikikandamiza kidogo. Nilijiuma ulimi. Nilibana tena miguu yangu kumzuia. Sikutaka aendelee hivyo ningechanganyikiwa. Nikajiachia tena. Hakunikopesha, alinipekecha, na kunisugua kwa ufundi, alinigusa na kunigusa na mwenzenu nikagusika. Nisingeweza kuendelea. Nilitamani nifanye zaidi ya hapo.

“Basi inatosha Freddy, siwezi zaidi nitapiga kelele” nilisema kwa sauti ya mnong’ono. Alikuwa ni kama amenibikiri. Nikapitisha mkono wangu kwenye mapaja yake na kumgusa. Toba yarabi! Alikuwa ametuna na tayari kwa mapambano. Nilimminya kidogo na kumpima, alikuwa amejaliwa. Wazo la yeye kuwa ndani yangu lilinipagawisha. Lakini tusingeweza kufanya lolote na mimi sikutaka kuendelea kukaa hapo muda mrefu zaidi.
“Asante Tina kwa kuja” alisema. Na mimi nilifurahi sana, nilichotamani ndicho kimetokea.
“Natamani nikuone tena Freddy” nilimuomba.
“Unafanya nini Jumamosi” aliniuliza.
“Nadhani nina ratiba tu za nyumbani sijui jioni itakuwaje”. Nilikuambia. Sikutaka kumuambia ukweli kuwa Jumamosi asubuhi nitakuwa na Waziri kwenye Uwanja wa Taifa kwenye sherehe za Muungano. Jioni Waziri alikuwa anaenda kwenye sherehe za chakula cha jioni Ikulu kusherehekea Muungano. Mimi sikuwa na mpango wa kwenda huko. Maana nikienda kwenye mikusanyiko ya namna hiyo ni kama nimeenda peke yangu kwani Waziri anazungukwa na wafu elfu moja wenye kutaka kusalimiana nao na wenye shida zao.
“Naweza kukurabisha kwangu Jumamosi jioni?” aliniuliza. Nilifikiria kwa haraka na kusema naweza anipatie maelekezo au tutawasiliana kesho yake Ijumaa kuthibitisha. Tukakubaliana tukutane Jumamosi kwake. Kwa vile hatukufika hapo pamoja tulisimama kuagana na tulikumbatiana kama marafiki tu bila kubusiana kabisa. Nilijisikia raha kuwemo katika mikono yake kwa sekunde hizo chache. Nilienda msalani na kujitengeneza na kunawa uso. Nilikuwa kama natembea kwenye mawingu, raha ilikuwa imeanza tu.

Nilipomaliza nilichukua gari yangu, na kwenda kujaza mafuta kwenye kituo cha mafuta cha BP kilichopo karibu kabisa na Blue Pearl Hotel. Baada ya hapo nilianza kukanyaga mafuta kuelekea Kiluvya. Jamani Mjamaika wangu.

Nilisubiri Jumamosi ifike haraka. Kesho yake Ijumaa nilipanga kwenda saloon ya Bantu iliyopo Kinondoni kwa ajili ya kujitengeza

nywele na kujiremba kwa ajili ya siku kuu ya Muungano. Wakati wengine walikuwa wanajiandaa na maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliounda taifa letu, mimi nilikuwa najiandaa kwa muungano mkubwa zaidi, muungano wa kukumbuka, muungano wa mimi na Mjamaika. Mwaka huu watakoma.

Ee Mola upe baraka!

Ngoja tuivuke Ijumaa.